

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname

Other names

**Pearson Edexcel  
International GCSE**

Centre Number

Candidate Number

--	--	--	--	--

--	--	--	--

**Thursday 21 May 2020**

Morning (Time: 2 hours 15 minutes)

Paper Reference **4SW1/01**

**Swahili**

**Paper 1: Reading, Writing and Translation**

**You do not need any other materials.**

Total Marks

### Instructions

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
  - Section A Questions 1–4
  - Section B Question 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)
  - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
  - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

### Information

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
  - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

### Advice

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

*Turn over ▶*

P62055A

©2020 Pearson Education Ltd.

1/1/1/1/



P 6 2 0 5 5 A 0 1 1 6



Pearson

**SECTION A: READING****Answer ALL questions.****Write your answers in the spaces provided.**

**Multiple-choice questions must be answered with a cross in a box ✕ . If you change your mind about an answer, put a line through the box ✕ and then mark your new answer with a cross ✕ . Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.**

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

**Matembezi ndani ya Jahazi**

Taarifa kwa watalii!

Tunapenda kuwataarifu kwamba sasa mtaweza kufanya matembezi ya kitalii ndani ya jahazi. Jahazi litasafiri katika Bahari ya Hindi kutoka eneo la Forodhani na kuzunguka magharibi ya kisiwa cha Unguja.

Ni muhimu kununua tiketi kwenye ofisi yetu kabla ya safari ili kuepuka kuchelewa. Tafadhal fika dakika ishirini kabla ya muda wa safari. Kwa sababu za usalama, kuna kikomo cha wasafiri watakaoruhisiwa kupanda jahazi. Mida ya safari ni saa nne asubuhi na saa nane mchana.

Mtakapokuwa jahazini mtaweza kuona mengi ikiwa ni pamoja na majumba muhimu huku mkisikiliza muziki asilia. Wapishi wetu hupika vyakula tofauti kila siku na mnakaribishwa kujipakulia wenyewe.



- |                   |                     |                  |                  |
|-------------------|---------------------|------------------|------------------|
| <b>A</b> onyo     | <b>B</b> kutembelea | <b>C</b> vivutio | <b>D</b> mapishi |
| <b>E</b> safari   | <b>F</b> ulinzi     | <b>G</b> vigumu  | <b>H</b> ushauri |
| <b>I</b> kulipa   | <b>J</b> kuogelea   | <b>K</b> Watalii | <b>L</b> nyingi  |
| <b>M</b> afadhali |                     |                  |                  |

<b>Example:</b>	Taarifa inawalenga...	<b>K</b>
<b>1 (a)</b>	Taarifa hii ni... kwa watalii.	
<b>1 (b)</b>	Kuna kikomo cha wasafiri kwa sababu ya...	
<b>1 (c)</b>	Ni... kununua tiketi kabla ya safari.	
<b>1 (d)</b>	Kuna... mbili za jahazi kila siku.	
<b>1 (e)</b>	Kutoka jahazini watu wanaweza kuona...	
<b>1 (f)</b>	... tofauti hutayarishwa kila siku.	

**(Total for Question 1 = 6 marks)**



P 6 2 0 5 5 A 0 3 1 6

- 2** Weka alama katika visanduku **10** vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

### Chakula shulenii

#### Fatuma



Siku hizi chakula kinachouzwa shulenii kwetu kinanivutia sana kina virutubisho vizuri. Zamani nilileta chakula changu mwenyewe kwani cha shule hakikuwa na ladha. Mimi sinunui kwa wachuuzi barabarani kwani siuamini usafi wao. Nimefurahi sana shule imegundua umuhimu wa lishe bora.

#### Lilian



Chakula kinachouzwa shulenii kwetu kimebadilika sana. Sasa tunaweza kuchagua chakula chenye afya zaidi. Tatizo pekee ni kwamba vyakula vingi huchemshwa tu na hivyo havina ladha nzuri. Kwa vile ninathamini afya yangu, mimi sili chakula cha wachuuzi. Ninakula ninaporudi nyumbani tu!

#### Yasini



Zamani shule yetu haikuwa na mgahawa. Sasa mgahawa wa shule unauzwa chakula kisichokuwa na ladha kwa bei ghali. Mimi ninapenda vyakula vilivyokaangwa na huvinunua barabarani kwa wachuuzi. Mama ananiambia niangalie afya yangu ingawa mimi simsikilizi kwani bado sijazeeka. Yeye hunitengenezea chakula kuchukua shulenii lakini huwa sili.

		Fatuma	Lilian	Yasini
<b>Mfano:</b>	Shule iliuza chakula zamani.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>A</b>	Hapendi chakula cha shule.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>B</b>	Anathamini afya yake sasa.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>C</b>	Huleta chakula cha nyumbani shuleni sasa.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>D</b>	Anavutiwa na chakula cha wachuuzi.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>E</b>	Ladha ya chakula shuleni ni mbaya.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>F</b>	Hula nyumbani tu.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>G</b>	Lishe bora ni muhimu kwa wazee tu.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>

(Total for Question 2 = 10 marks)



- 3** Soma makala kuhusu Ajira ya Hannah. Malizia taarifa kwa kutumia nambari au maneno kwa **Kiswahili**.

### Ajira

Baada ya kuhitimu masomo yake ya udaktari, Hannah aliwaarifu wazazi wake kwamba yeeye angependelea kusafiri kwa mwaka mmoja kabla ya kuanza kazi hospitalini. Baba yake alimwuliza ‘umehitimu baada ya kusomea udaktari kwa miaka saba na unataka kusafiri?’ Baba yake alisisitiza kwamba angependelea kama Hannah angebakia Nairobi na kutafuta kazi. Hannah alimweleza kwamba alihitaji kusafiri ili kuiona dunia na kupumzika baada ya kazi kubwa ya kusomea udaktari.

Ili kuwafurahisha wazazi wake, Hannah aliamua kutafuta kazi itakayomruhusu kusafiri. Alituma maombi kwenye kampuni ya usafirishaji watalii ambayo ingemwezesha kutembelea mahali tofauti na pia kupanda milima iliyopo Afrika ya Mashariki. Hannah hakutegemea kupata kazi hiyo kwani hakuwa na uzoefu na hakuwa na mwili uliozoea mazoezi. Alishangaa sana alipopata kazi hii.

Alipokuwa kazini alitambua kwamba kampuni ilimchagua kwani ilihitaji daktari safarini. Mwishoni Hannah aliifanya kazi hii kwa miaka minne akifurahia kuwatibu watalii walioumia huku akijenga uzoefu.



**Mfano:** Hannah amesomea: ..... **udaktari** .....

- (a) Tamaa ya Hannah: ..... (1)
- (b) Muda uliochukuliwa kwa masomo: ..... (1)
- (c) Mji anaoishi Hannah: ..... (1)
- (d) Sababu za kutaka kusafiri: ..... na ..... (2)
- (e) Maoni ya baba kuhusu kusafiri: ..... (1)
- (f) Faida za kazi yake: ..... na ..... (2)
- (g) Changamoto za kuajiriwa: ..... na ..... (2)
- (h) Hisia ya kuajiriwa: ..... (1)
- (i) Sababu ya kuajiriwa: ..... (1)

**(Total for Question 3 = 12 marks)**



P 6 2 0 5 5 A 0 7 1 6

- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kitiwacho **Kiu**, kilichoandikwa na Mohamed S. Mohamed.

### Bahati

Mwinyi alikuwa ameketi chumbani kwake, chumba alichopenda kupumzikia. Chini ya nyayo zake alikuwa amekanya zulia zuri ambalo thamani yake ingetosha kumfariji maskini kwa siku na miezi. Madirisha yake yalifungukia katika kitalu cha miti ya maua aliyoyatunza kwa uangalifu. Haya yalichanua kwa nyakati mbalimbali na kubadili mandhari na harufu ya mahali pale kila mara.

Mbali na alipokuwa Mwinyi aliishi Bahati. Bahati aliporejea kwao hakumkuta mama yake nyumbani. Alikuwa amekwenda kwa jirani kutwanga mchele wake kwa ajili ya biashara yake ya vitumbua alivyoviiza barabarani. Mama yake alichukia kuomba misaada kwa majirani na hamu yake ilikuwa kununua kinu na mchi wake mwenyewe. Hakuwa na uwezo. Mara kwa mara alisema ‘kila ninapogonga milango, ninakumbushwa kuwa *uso wa binadamu hauwezi kuficha haya*’.

Siku hiyo, Bahati alihisi furaha na matumaini kwa wakati ujao. Ilikuwa bahati mbaya kwamba mama yake hakuwapo nyumbani kusikia habari yake njema. Alikuwa na hamu ya kumweleza kuhusu Mwinyi na kwamba sasa hatakuwa na haja ya kuuza vitumbua, ataupitisha uzee wake katika raha ya nyumba nzuri.

Baada ya kuwaza hivi Bahati alitoka hima akamfuata mama yake kwa jirani ambapo alimpokea mchi na kuanza kutwanga huku akitabasamu.

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

(a) Mahali gani humpa Mwinyi furaha anapokuwa nyumbani?

(1)

(b) Nini umuhimu wa zulia kwenye habari uliyoisoma?

(1)

(c) Maua yana maana gani katika habari hii?

Toa maelezo **mawili**.

(2)

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



(d) Tunajuaje kwamba mama yake Bahati si tajiri?  
Toa maelezo **mawili.**

(2)

(e) Mama yake Bahati ana ndoto gani?

(1)

(f) Nini maana ya '*'uso wa binadamu hauwezi kuficha haya'* kwenye habari hii?

(1)

(g) Bahati ana mipango gani kuhusiana na mama yake?  
Toa maelezo **mawili.**

(2)

(Total for Question 4 = 10 marks)

**TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS**



P 6 2 0 5 5 A 0 9 1 6

**SECTION B: WRITING**

Answer Question 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)

**Write your answers in the spaces provided.**

**5****Matumizi ya simu**

Simu

Rafiki

Mwaka uliopita

Kesho

Andika takriban maneno **70** kwa **Kiswahili** kuhusu Matumizi ya simu. Ni lazima kutumia maneno yote yaliyotajwa hapo juu.

**(12)**

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 5 = 12 marks)



P 6 2 0 5 5 A 0 1 1 1 6

- 6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika takriban maneno 130 kwa **Kiswahili**.

### Chaguo 1

(a)



Andika makala kuhusu matumizi ya intaneti kwa vijana. Ni lazima uandike kuhusu:

- Intaneti shulenii kwako
- Faida na/au hasara za intaneti
- Matumizi yako ya intaneti.

(20)

### Chaguo 2

(b)

Mama yangu ameniambia kwamba mtahamia kwenye mji mwengine  
mwezi ujao. Je, una hisia gani?

Rafikiyo,

Fauzia

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Utakumbuka nini katika maisha yako sasa
- Mawazo yako kuhusu nyumba yako mpya
- Hisia zako kuhusu kuhamia kwenye mji mwengine.

(20)



**Chaguo 3**

(c) Ulialikwa kwenye sherehe ya harusi nchini kwako hivi karibuni. Kwenye ukurasa wako wa blogu andika:

- Maelezo kuhusu bibi na bwana harusi
- Elezea mahali ambapo sherehe imefanyika
- Tukio la kuchekesha harusini.

(20)

**Indicate which question you are answering by marking a cross . If you change your mind, put a line through the box  and then indicate your new question with a cross .**

 **Question 6(a)** **Question 6(b)** **Question 6(c)**

P 6 2 0 5 5 A 0 1 3 1 6

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**(Total for Question 6 = 20 marks)**

**TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS**



**SECTION C: TRANSLATION INTO SWAHILI****Write your answer in the space provided.**

- 7 Tafsiri aya ifuatayo kwa **Kiswahili**.

**Film Festival**

The Zanzibar International Film Festival is East Africa's largest film, music and arts festival. For two whole weeks, it brings together new talent from all over the world. Each year, some of the most captivating films are screened in venues across the island. Films are submitted based on a yearly theme and they are then entered into competitions. The final night is an awards night where the winning films are celebrated.

---

**(Total for Question 7 = 10 marks)**

---

**TOTAL FOR SECTION C = 10 MARKS**  
**TOTAL FOR PAPER = 80 MARKS**

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

## BLANK PAGE

### Source information

#### Question 2

- © michaeljung/Getty Images
- © SDI Productions/Getty Images
- © Motortion/Getty Images

#### Question 6

- © Getty Images

